

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA IDARA YA AFYA
MAENDELEO YA JAMII JINSIA WAZEE NA WATOTO;
KITENGO CHA MAGONJWA YALIYOKUWA HAYAPEWI
KIPAUMBELE**

Taarifa ya unyweshaji dawa Shuleni kwa Mkuu wa Wilaya 02/05/2015

Mh Mkuu wa wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa iliingizwa kwenye mpango huu wa kutoa kinga tiba ya Magonjwa yaliyokuwa hayapewi Kipaumbele tangu mwaka 2010 kwa dhumuni la kupambana na Magonjwa hayo.

Kwa kuwa Magonjwa haya ni mengi Wizara iliamua kuyapanga Magonjwa haya katika makundi yanayoweza kudhibitiwa kwa namna moja na kushirikisha kada tofauti katika kuyadhhibiti Magonjwa haya. Mfano Magonjwa kama:

- I. Matende na Mabusha
- II. Trakoma au Vikope
- III. Minyoo ya tumbo
- IV. Kichocho na usubi

Magonjwa haya yatadhhibitiwa na waalamu wa tiba kwa kutoa dawa katika jamii, hali kadhalika Maafisa wa Afya watasaidia kuhamasisha ujenzi na matumizi sahihi ya vyoo pamoja na kuangamiza (vector) wadudu wanao sambaza Magonjwa haya toka kwa jamii/sehemu moja kwenda nyingine.

Hivyo magonjwa kama Kichaa cha mbwa, Ukoma na Magonjwa mengine ambayo hatujayataja ,hudhibitiwa kwa njia nyingine na katika vitengo maalumu.

TAARIFA ZA DAWA

2016

MAELEZO	ZOEZI	KE	ME	JUMLA
Idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule walengwa Kutoka katika rejesta zote 2	School MDA	39,843	35,975	75,818
Idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule miaka 5 hadi 14 ambao wamepatiwa tiba kinga jumla kutoka kwenye rejesta zote	School MDA	38,891	35,919	74,810
Coverage	School Mda	98 %	98 %	98 %

2017

MAELEZO	ZOEZI	KE	ME	JUMLA
Idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule walengwa Kutoka katika rejesta zote 2	School MDA	41,673	36,043	77,519
Idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule miaka 5 hadi 14 ambao wamepatiwa tiba kinga jumla kutoka kwenye rejesta zote	School MDA	40,231	34,667	74,898
Coverage	School MDA	99.7%	99.7%	99.7%

2018

MAELEZO	ZOEZI	KE	ME	JUMLA
Idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule walengwa Kutoka katika rejesta zote 2	School MDA	40,817	36,935	77,752
Idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule miaka 5 hadi 14 ambao wamepatiwa tiba kinga jumla kutoka kwenye rejesta zote	School MDA	39,924	36,043	75,967
Coverage	School Mda	97%	97%	97%

HALI HALISI KWA MWAKA 2018/19

Mhe. Mkuu wa wilaya hali halisi ya Magonjwa katika Wilaya yetu kwa mujibu wa takwimu za hospitali inaonesha kuwa bado hali ya ugonjwa wa Macho na Minyoo ni miongoni mwa Magonjwa kumi yanayoisumbua jamii ya Wakazi wa Mpwapwa, licha ya jamii / watoto wa shuleza msingi kunywa dawa kwa kipindi chote hicho, baadhi ya sababu ya kuendelea kwa maradhi haya ni:

- Baadhi ya wana jamii kuwa na uwelewa mdogo kuhusu Magonjwa haya, lakini pia kutokuwa na imani na Dawa wanazopatiwa Shuleni na katika Jamii hivyo kubaki na vimelea vya Magonjwa hayo na kuvisambaza tena katika jamii mara baada ya matokeo mazuri kuonekana.
- Baadhi ya wanakaya kutozingatia kanuni za usafi wa Mazingira ujenzi na matumizi sahihi ya vyoo bora.
- Baadhi ya kaya /jamii kutomeza dawa kwa miaka mitano mfululizo hivyo kukatisha dawa kwa mwaka mmoja au miwili hutoa nafasi kwa vimelea kuendelea kuwapo Mwilini.

UFUMBUZI;

- Kuendelea kulelimisha jamii juu ya madhara inayoweza kupata kwa kutomeza dawa hizi kwa usahihi
- Kutoa elimukwa jamii inayohusiana na magonjwa haya kwa kupitia wataalamu mbalimbali waliopo katika maeneo yote ya mijini na vijijini kwa kutumia mbinu mbalimbali mfano picha za waathirika wa magonjwa haya ,vipeperushi na vijitabu vinavyoelezea magonjwa haya

MWISHO;

Mh Mkuu wa Wilaya tunapenda kutoa pongezi zetu za dhati Kwako,kwa kukubali kushiriki katika zoezi hili maalumu la kutuzindulia siku ya unyweshaji dawa katika shule zote za msingi kwa watoto kuanzia miaka Mitano hadi kumi na Nne waliopo na wasiopo katika shule za Halmashauri yako.

Asante;